TANZANIA / JUDGMENT

african foundation for education dhidi ya ramadhani mchatta na wenzake 6 2021 tzhcld 117 23 aprili 2021

COURT
TANZLII

DECIDED
1 January 2021

Source: media.tanzlii.org · Research copy typeset by Esheria. Not court-issued or certified.

MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DIVISHENI YA KAZI PAR ES SALAAM MAOMBI YA MAREJEO NA. 808 YA 2019 KATIYA AFRICAN FOUNDATION FOREDUCATION..... MUOMBAJI DHIDIYA RAMADHANI MCHATTA NA WENZAKE 6..... ..^WAJIBU MAOMBI HUKUMU < Tarehe ya Amri ya Mwisho: 17/03/2021 Tarehe ya Hukumu: 23/04/2021 v-. Aboud. J. ■' Katika shauri hili mupmbaji anaipmba Mahakama kufutilia mbali uamuzi wa kushikiliaamri. ya^kusikiliza shauri upande mmoja katika mgogoro Na. GMA/DSM/ILA/487/2019 uliyotolewa na Tume ya *■?' ■— _ V Usuluhishi 'na' Uamuzi '(itakayorejewa kama Tume). Maombi haya (/~Ss-X.^' yameletwa^chini ya kifungu cha 91 (1) (a) cha Sheria ya Ajira na Mahusiaqo/Kazini, [SURA 366 KM 2019] (itakayorejewa kama Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini), Kanuni ya 24 (1), 24 (2) (a) (b) (c) (d)

(e) (f), 24 (3) (b) (c) (d), za Kanuni za Mahakama ya Kazi, Tangazo la Serikali Na. 106 la 2007 (Katika maamuzi haya itarejewa kama Kanuni za Mahakama ya Kazi). i Wajibu maombi hawakuleta kiapo kinzania wala kuhudhuria katika shauri hili, hivyo Mahakama iliendelea kusikiliza na kuamua shauri hili upande mmoja kama ilivyoelekezwa katika Kanuni 37 (1) ya Kanuni za Mahakama ya Kazi. Shauri hili pia liliendeshwa kwa njia ya maandishi na muombaji aiiwakilishwa na Wakili Said M. Seif kutoka Kampuni ya Mawakili ijulikanayo kwa jina laZJ. Advocates. Katika shauri hili muombaji anaomba".kutengua' rnaamuzi ya Tume kwa sababu kuu mbili zifuatazo:-

i. Kwamba hakukuwa na .. usfiahidjfe. wowote uliotolewa kuthibitisha kuwa muombaji 'alifikishiwa hati ya wito zaidi tu ya maelezo ya wajibu maombi. ii. Kwamba tarehe., ■•11/07/2019 katika mgogoro Na. -.X. 'w CMA/DSM/ILA/487/2019 muombaji akizuiliwa na tukio ambalq hakulitarajia hivyo muombaji alishindwa kufika mbele ■si-z s s ' - ya^Tupe kwa wakati. Wakili wa muombaji akitoa maelezo yake katika hoja ya kwanza katika shauri hili, aliieleza Mahakama kuwa, muombaji hakupewa hati ya wito kama inavyodaiwa na wajibu maombi na hakuna ushahidi wowote wa kuthibitisha hilo. Wakili huyo aliendelea kueleza kuwa muombaji alipokea hati ya wito tarehe 02/07/2019 na tarehe 2 11/07/2019 alimtuma wakili wake kumuwakilisha katika mgogoro huo jambo ambalo asingefanya kama alikua na nia ya kukataa wito. Wakili huyo aliongeza kuwa taarifa za kukataa kupokea wito

ni nia ovu iliyotengenezwa na wajibu maombi kwa lengo la kumnyima muombaji haki ya kusikilizwa kinyume na Ibara 13 (6) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, [SURA 2 KM 2002]. , •* s\ j * Katika hoja ya pili ilielezwa kuwa tarehe 11/07/2019 siku - iliyokuwa imepangwa kusikiliza mgogoro.... niio, wakili wa muombaji alipata matatizo ya kifamilia, kwamba jtuna'^idugu yake alimpeleka hospital! hivyo alimuomba wakili mwenzake Bw. Mohamed Nyenye !} aweze kumuwakilisha katika mgogoro huo. Aliendelea kuelezwa kuwa wakati anapewa. maagiza wakili Mohamed Nyenye naye alikuwa na kesi Mahakarria Kuu, Masjala Kuu alipokuwa akihudhuria Kesi Na. Misc. Civ.App.l. Nd: 775/2015, Mohamed Builders v. Adam Said, iliyokuwa imbele ya Mhe. Massam, Naibu Msajili iliyosababisha achelewe'kufika Tume. Aliendelea kuelezwa kuwa, muwakilishi wake alipofika Tume alikuta tayari amri ya kusikiliza shauri upande mmoja imeshatolewa. Wakili wa muombaji aliongeza kuwa muombaji alieleza sababu za msingi na za kutosha kutengeu amri ya kusikiliza shauri upande 3 mmoja. Hi kuyapa nguvu maelezo yake muombaji alirejea maamuzi mbalimbali zikiwemo, kesi ya Abdalah Zarafi Vs. Mohamed Omari

(1969) HCD p. 347-348, Mkurugenzi Tarime Goodwill Foundation Vs. Editha Salongo Tibamanya, Rev. No. 23 ya 2019 HC Musoma. Kutokana na maelezo hayo hapo juu vyakili^ wa \mupmbaji aliiomba mahakama hi! ikubali maombi yake ya kutehgua amri ya kusikilizwa shauri upande mmoja. , X'. X-? Baada ya kupitia hoja . za muombaji,Xsheria mbalimbali na f v, kumbu kumbu za mahakamaX naona -mahakama hii inajukumu la

- *J kutatua hoja hii, kuwa je'rnuombaji alieleza na kuthibitisha sababu za **\ 1* msingi za kushindwa kufika Turne? Sababu (kuu'aliyditoa muombaji ya kushindwa kufika Tume i/x\ j' kama ilivyopangwa ni kwamba tarehe ambayo kesi ilikuwa imepangwazwakili wake aliuguliwa na ndugu yake hivyo kuwajibika kumpeleka hospital!. Lakin! wakili huyo hakuleta uthibitisho wowote kuwa alienda hospital! siku hiyo. Aidha, hata sababu ya kuwa muwakilishi wa wakili huyo alikuwa na kesi Mahakama Kuu, Masjala kuu kama ilivyotajwa hapo juu naona pia haijathibitishwa kwani hakuna nakala yoyote iliyotolewa kuthibitisha uwepo wa kesi hiyo. 4 Muombaji pia amesema hakuna uthibitisho wowote wa kupelekewa hati ya wito. Hata hivyo, ukipitia jalada la Tume kuna stakabadhi za posta ambapo muombaji huyo alitumiwa wito mara tatu hata hivyo alishindwa kuhudhuria Tume. Katika mazingira hayo, naona kuwa muamuzi alikuwa sahihi kuendelea na amri ya kusikiliza shauri upande mmoja kwani muombaji hakutoazsababu,\zozote za msingi na zenye mashiko za kushindwa kuhudhuria mbele'ya Tume katika mgogoro huu. , ,; ' x... Hata hivyo, baada ya kupitia -mwenehdo'wa Tume nimeona kuwa maamuzi ya kukataliwa kuterigua^amri ya kusikilizwa shauri upande mmoja yalitolewa>tarehe.:16/10/2019. Na ilipofika tarehe 23/10/2019 muombaji aliwasilisha maombi yake hapa mahakamani akikuomba kuteriguliwa kwa maamuzi ya kusikiliza shauri upande mmoja. Madmbi haya mbele ya mahakama hii hayakuizuia Tume

- "v V'- —•' > kuendelea (■kusikiliza shauri hilo upande mmoja kama ilivyokuwa imeamuriwa. Hivyo basi, Tume iliendelea kusikiliza shauri upande mmoja na tarehe 08/11/2019 Tume iliyafutilia mbali maombi ya wajibu maombi ya kuomba kufungua shauri nje ya muda kwani

hawakueleza sababu za msingi za kuchelewa kufungua mgogoro wao. Katika mazingira ya 5 shauri hili, ni mtazamo wangu kuwa maombi ya muombaji yamepoteza nguvu au hayana mantiki kwani anaomba kutengua amri ambayo tayari imeshafanyiwa utekelezaji. Kwa maneno mengine maombi ya wajibu maombi tayari yalikwishasikilizwa na Tume upande mmoja na yalitupiliwa mbali tarehe 08/11/2019 kama ilivyoelezwa hapojuu. , ? ' \ Kutokana na sababu zilizoainishwa hapo-. juu, Mahakama hii inayathibitisha maamuzi yaliyotolewa na Tume 'ya kuendelea na shauri upande mmoja kama yalivygtolewa. tar.ehe 08/11/2019 katika Mgogoro Na. CMA/DSM/ILA/487/2019. Jbiiyyo basi, maombi haya ya marejeo yanatupiliwa mbali? / Imeamuriwa,hivyo, ’ ?■> J D. Aboud 23/04/2021 6

Source & reproduction note

Judgment wording, source notices and original paragraph numbers are retained. Esheria supplies the layout and this PDF’s page numbers; these are not the source pagination. This is a research copy, not an official or certified court document. Check quotations, citations and publication restrictions against the original source before relying on it.

ORIGINAL SOURCE https://media.tanzlii.org/media/judgment/155077/source_file/african-foundation-for-education-dhidi-ya-ramadhani-mchatta-na-wenzake-6-2021-tzhcld-117-23-aprili-2021.pdf

CASE PAGE https://chat.esheria.ai/case-law/tanzania/Expartehearing-tanzlii-2021--6a3ea52a3b1caa9129823287

Prepared on 29 October 2026 · Esheria